JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE
SHULE YA SEKONDARI INYONGA

Namba za simu
Mkuu wa Shule 0757682461/0787137188
Makamu Mkuu wa Shule 0746133240/0748449432

SHULE YA SEKONDARI INYONGA,
S.L.P. 46,
MPANDA-KATAVI.

01/042022

Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi……
SLP……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022

1. Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano, katika shule hii mwaka 2022.Shule ya sekondari Inyonga ni ya bweni na nimchanganyiko wa wavulana na wasichana.Shule ipo makao makuu ya wilaya ya Mlele Mkoa wa Katavi.

   Shule itafunguliwa muhula wa kwanza tarehe……/……../ 2022

   Hongera kwa kuchaguliwa katika shule hii.Ninakutakia maandalizi mema na safari njema.

   Karibu Sana Shule ya Sekondari Inyonga.

……
PAT RICK U. KAPITA
(M KUU WA SHULE)

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

A. USAFIRI

Kila Mwanafunzi atajitegemea usafiri. Usafiri wa basi kutoka mjini Mpanda kuja Inyonga-Mlele unapatikana katika kituo cha mabasi kilichoko Mpanda na kutoka mjini Tabora kuja inyonga unapatikana mjini Tabora. Kutoka kituo cha mabasi Inyonga kuja shuleni kuna umbali wa km 2 na pia kuna usafiri wa bodaboda na bajaji.

B. SARE YA SHULE

1. WASICHANA

I. DARASANI

a) Sketi za darasani mbili, rangi ya miraba (draft) ya khaki, linda ndogo moja (1) na rangi ya udongo moja (1), mshono wa solo (kukata)(ndefu inayofika kwenye kisigino).
b) Fulana (T-shirt) ya darasani rangi ya bluu yenye nembo ya shule.
c) Shati nyeupe jozi mbili zenye mikono mirefu isiyo na urembo wowote. Wanafunzi wa kiislamu washone nusu kanzu nyeupe itakayoambatana na hijabu yake.
d) Viatu vya shule ni vyeusi vyenye visigino vifupi (simple shoes) jozi mbili.
e) Soksi nyeupe jozi mbili.
f) Sweta moja rangi ya kijani choroko (mpauko).

II. KAZINI

a. Sketi ya kushindia (Shamba dress,) rangi nyekundu ya miraba (draft) ndogondogo mshono wa solo ndefu inayofika kwenye kisigino, na T-shirt ya kushindia (Shamba dress) rangi kijivu, yenye nembo ya shule. Wanafunzi wa kiislamu washone nusu kanzu ya kijivu na hijabu ya rangi ya kijivu inayofanana na nusu kanzu.
b. Soksi nyeusi kwa ajili ya kushindia.
c. Bajaji nyeusi kwa ajili ya kushindia.

III. SAFARINI

a. Mwanafunzi anapokuwa safarini au nje ya shule atavaa T-shirt ya bluu yenye nembo ya shule na sketi drafti ya khaki.
b. Kwa waislamu watavaa sketi ya khaki na nusu kanzu na hijabu rangi ya kijivu

IV.MICHEZO

a.Sketi ya michezo rangi ya light blue na T-shirt ya rangi nyekundu yenye nembo ya shule.

b.Atavaa raba nyeupe wakati wa michezo.

2. WAVULANA

I.DARASANI

a. Suruali mbili za darasani, rangi ya khaki na rangi nyeusi.
b. Shati nyeupe jozi mbili mikono mirefu isiyo na urembo wowote.
c. T-shirt ya darasani 1, rangi ya blue yenye nembo ya shule.

d. Viatu vya shule, vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili.
e. Soksi jozi mbili nyeusi.
f. Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi.
g. Sweta moja rangi ya kijani choroko (mpauko).

I. KAZINI

a. Suruali ya kushindia (shamba dress) rangi ya udongo.
b. T-shirt ya kijivu yenye nembo ya shule kwa ajili ya kushindia.
c. Aje na raba nyeusi kwa ajili ya kushindia.

II. SAFARINI

a. Mwanafunzi anapokuwa safarini au nje ya shule atavaa T-shirt ya bluu yenye nembo ya shule na suruali ya khaki na viatu vya darasani.

III. MICHEZO

a. Sare ya michezo kwa shule hii ni raba rangi nyeusi, bukta rangi ya kijani na T-Shirt moja rangi nyekundu.

IV. MAANDALIO YA KUSOMA

a. Track suit jozi moja rangi ya blue kwa ajili ya maandalio ya kusoma.

ANGALIZO: **Si jukumu la Shule kushona sare za wanafunzi, Mwanafunzi husika ataelekezwa kwa mtu aliyeteuliwa na shule kwa kazi hiyo, utaratibu huu umewekwa ili wanafunzi wawe na sare zinazofanana. Kama mzazi ataamua kumshonea mtoto wake sare yoyote, na rangi au mshono ukawa tofauti na shule, basi mzazi atalazimika kumshonea sare nyingine kwa maelekezo ya mwalimu muhusika shuleni.**
Fedha ya sare za shule aje nayo mkononi, atakabidhiwa fundi.

NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA MAVAZI YA AINA YOYOTE ZAIDI YA SARE ZILIZOTAJWA HAPO JUU.

C. ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 pia unaweza kulipa nusu kiasi cha shilling 35,000.00kwa muhula.
b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-
   i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
   ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho.
   iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma kwa mwaka.
   iv. Shilingi 30,000/=kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
   v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule.
   vi. Shilingi 10,000/=(kwa mwaka)kwa ajili ya matibabu, ambapo 5000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na Tsh 5000/= kwa ajili ya Bima ya Afya (CHF).***Tafadhari ii kuepuka usumbufu fedha hii ya matibabu mwanafunzi afike nayo shule na ataikabidhi kwa mtunza fedha.***

vii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima mock.

viii. Mwanafunzi aje na godoro la futi $2^1/_2$kwa 6 kwani shule haina magodoro ya kukodisha.Magodoro ya kununua yanapatikana hapahapa mjini.

ix. Fedha ya tahadhari 5000/= (haitarejeshwa).

NB. Ada na michango iliyotajwa katika kifungu A na B hapo juu isipokuwa fedha ya matibabu ilipwe kwenye Akaunti ya shule Na 61901200067 katika Benki ya NMB jina la akaunti ni INYONGA SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT (Tafadhali **andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na aje nayo shuleni**)

D. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

a. Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)

b. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

Kwa sababu shule ina uhaba wa vitabu,ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo (tahasusi) husika

I. VITABU VYA KEMIA:-

1. BY S. chand, Conceptual Chemistry for class XI and XII
2. By Tanzania Institute of Education, ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY part I and II.
3. Advanced chemistry Review (2000 -2012)

II. VITABU VYA BIOLOJIA:-

1. Dissecting kit – kwa ajili ya practical
2. Laboratory coat kwa ajili ya mazoezi ya vitendokwa wanafunzi wa Sayansi
3. By Taylor at el (1999) Biological Science, third edition. Tong printing press Hong kong.
4. By Glenn and Tod,s (1999) Understanding Biology 4th Ed.Stanlye Thomes Ltd UK.

III. VITABU VYA UCHUMI:-

1. C.M. Ambilikile – Advanced level paper two and professional studies
2. Economic 2; Advanced levels paper two and professional studies
3. Economic simplified (revised and update)
4. Undestanding Economics (Remed H. Chegee.M)

IV. VITABU VYA JIOGRAFIA:-

1. Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman.
2. Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D
3. Pritchard J.M. (1990) practical Geography for Africa Longman.
4. Kamili, 2, physical Geography for Africa Dar es salaam Afroplus Industries.
5. Msabila D.T. Physical Geography Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
6. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambali Nyangwine publishers.

V. VITABU VYA KISWAHILI

1. Kiswahili 1. Christopher masuko, kidato cha tano nadharia ya lugha
2. Tahakiki kidato cha tano na sita
3.Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II
4. Vitabu fasihi

Riwaya : Vuta ni kuvute, Mfadhili, Usiku utakapokwisha na Kufikirika.
Tamthiliya: Ukingo wa thimu, Nguzo mama, Kivuli kinaishi na Morani
Ushairi : Kimbunga, Fungate ya uhuru, Chungu tamu na Mapenzi
5.Miundo ya Kiswahili sanifu kilichoandikwa na Samikisa
6. Nadharia ya lugha ya Kiswahili kilichoandikwa naP. saluhaya

VI. VITABU VYA HISTORY

1. By Webster J.B. The growth of African Civilization, the revolutionary years of West Africa since 1800, longman press

2. How Europe underdeveloped Africa.

VII. VITAVU VYA ENGLISH LANGUAGE

1. Nyambari nyangwine 2010 advanced level Literature
2. Francis mnyari (2014) advanced level English
3. POEMS TIE. SELECTED POEMS NA WONDERFUL SURGEION BY CHARLES MLOKA
4. Plays: I WILL MARY WHENI I WANT, LWANDA MAGERE,NA BETRAYAL IN THE CITY NA AN ENEMY OF THE PEOPLE
5. Novel: A MAN OF THE PEOPLE, A BEATIFULY ONE ARE NOT YET BORN NA HIS EXCELENCY THE HEAD OF THE STATE

VIII.GENERAL STUDIES:-

1. General studies Approach.

IX ADVANCE MATHEMATICS

1.S Chands Class XI&XII
2. Scientific calculator zinapatikana shuleni kwa bei nafuu
3.Understanding Mathematics

VYOMBO VYA CHAKULA

a. Sahani, bakuli na kijiko.
b. Kikombe(chenye ujazo wa nusu lita) na bakuli.

VITENDEA KAZI

a. Scientific calculator.
b. Madaftari makubwa yasiyopungua saba
c. Mwanafunzi wa tahasusi ya CBG, aje na dissecting kit, stop watch na tray.
d. Mashuka pair 2 rangi kijani, blanketi 1 foronya 1 chandarua 1.
e. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa matumizi ya mwanafunzi na shule.
f. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio ya ndani (soft broom) na nje(chelewa) na mopa 1 , hard brash.

MWANAFUNZI LAZIMA AJE NA RESULTS SLIP YA MATOKEO YAKE YA KIDATO CHA NNE ORGINAL NA SIO KIVULI ASIPOKUJA NAYO HATAPOKELEWA NA KIVULI CHA CHETI CHA KUZALIWA.

E. SHERIA ZA SHULE

1. MIPAKA YA SHULE

a. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vijiji jirani wala kwenda mjini bila kibali cha mkuu wa shule.
b. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini ya mkuu wa shule.
c. Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana kwenye idara za masomo baada ya saa 12 jioni.

2. UTARATIBU WATIKA WA CHAKULA.

a. Ni lazima kufuata taratibu na saa zilizopangwa za kula kulingana na utaratibu wa shule.
b. Kila mwanafunzi awe na sahani, bakuli, kijiko na kikombe. Vyombo hivi vitunzwe bwenini.

c. Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wa chakula.
d. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na ndala au kiatu cha wazi ndani ya eneo la chakula.

3. JIKONI

a. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia jikoni wala kujipikia anavyotaka.
b. Viongozi wa zamu na viongozi wa chakula ndio wanaoruhusiwa kuingia jikoni wakati wa kupakua.

4. MABWENINI

a. Wanafunzi hawaruhusiwi kulala bwenini wakati wa vipindi.
b. Kila mwanafunzi ni lazima alale katika bweni na chumba alichopangiwa.
c. Ni marufuku kupiga na kusikiliza mziki bwenini.
d. Uharibifu/upotevu wa mali ya umma bwenini utalipwa na wakazi husika wa bweni.
e. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia au kula chakula bwenini.
f. Mwanafunzi azingatie usafi siku zote.

5. DARASANI

a. Wanafunzi waingie kwa wakati darasani kulingana na ratiba ya shule.
b. Mwalimu anapoingia darasani wanafunzi wasimame na kumuamukia.
c. Wanafunzi wasipige kelele wawapo darasani.
d. Wanafunzi wasitoke nje ya darasa bila ruhusa maalumu.
e. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuuliza na kujibu maswali na kukamilisha kazi alizopewa.
f. Usafi wa darasani ni wajibu wa kila mwanafunzi.

6. NJE YA DARASANI

a. Wanafunzi wasimame na kusalimia mwalimu au mtu aliyewazidi umri anapopita.
b. Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni kama inavyostahili.
c. Wanafunzi watumie lugha ya heshima kwa walimu, watu wengine na hata wao kwa wao.
d. Wanafunzi wawe na moyo wa kusaidaina na kushirikiana wakati wa shida na raha.
e. Mwanafunzi ataongea lugha ya kingereza wakati wote awapo shuleni.

7. MATIBABU

a. Wagonjwa wote watatibiwa katika hospitali ya serikali ya wilaya.
b. Shule itagharimia matibabu kwa gharama ya hadi elfu **25,000/=** tu na zaidi ya hapo mzazi au mlezi atalazimika kuongeza gharama zitakazoongezeka.

8. WAGENI

a. Wageni wa aina yoyote hawaruhusiwi kuingia au kupita shuleni bila shida au idhini ya mlinzi.

b. Wageni wa aina yoyote ile hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi isipokuwa kwa wale wenye shida za kiofisi tu.
c. Maagizo yote ya wageni kwa wanafunzi yatapokelewa na mwalimu wa zamu au makamu mkuu wa shule kwa maandishi.

9. HUDUMA ZA OFISI

a. Ofisi itapokea taarifa za dharura za wanafunzi kama vile msiba au tatizo kubwa la kifamilia pamoja na maagizo yote ya wazazi/walezi.
b. Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupokea simu bila idhini ya Mkuu wa shule.
c. Barua za wanafunzi zitapokelewa na mwalimu wa zamu na kupelekwa kwa wanafunzi na kiranja wa zamu.
d. Siku za mawasiliono itakuwa siku za mwisho wa wiki tu..

F . MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi:
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

Elewa si rahisi kutunga sheria za kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi.

“ELIMU NI MAISHA’’

G.VIAMBATA NA FOMU MUHIMU

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mgangaMkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni, kulipa ada, Michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

d) Picha nne (4) paspot size za Mwanafunzi na namba za simu nne za Wazazi na Nduıgu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumsaidia inapotokea shida

H.TAFADHALI SOMA KWA MAKİNİ MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

.

Saini ya Mkuu wa Shule……. .....

Jina la Mkuu wa Shule…….. PATRICK U KAPITA

Mhuri wa Mkuu wa Shule…… le.....THE HEADMASTER.....

KIAMBATA 'A`

INYONGA SECONDARY SCHOOL,
P . O. BOX 46,
MPANDA-KATAVI

FOR MEDICAL EXAMINATION
To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants
Student's full name …….
Age …… Years …….. Sex ……..
Blood count (red and whites) ……..
Stool examination ……..
Urine analysis
Syphilis and other venereal diseases test ……
……
T.B test ……
Eye Test …….
Ears ……..
…….
Abdomen ……
Urine for plant test …….

ADDITIONAL INFORMATION
Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc
……
….
……
….
I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education
Station ……..... Signature …….
Date. …… Designation ……..

KIAMBATA 'B'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE
SHULE YA SEKONDARI YA INYONGA

Kumbukumbu Namba: INY/SS/ADI/49/2016/……

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII:-

A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba …….. Hai/Si hai
2. Jina la Mama …….. Hai/ Si hai
3. Kama Baba si hai/ni hai jina la mlezi ni …….
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi ……..
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi……
6. Uraia wa wazazi

-Baba Mtanzania/Si Mtanzania
-Mama Mtanzania/ Si Mtanzania

7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi unataka aende wapi?

……..

8. Jina la mtu aendako ……..

Uhusiano na motto/mwanafunzi.

……. ……..

SAHIHI YA BABA/MLEZI ……. SAHIHI YA MWANAFUNZI……

TAREHE …….. TAREHE …….

KIAMBATA 'C'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE
SHULE YA SEKONDARI INYONGA

FORMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi …… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa
kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa
wameshindwa ila kwa sababu ni chache.
Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Inyonga. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule.
Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.
Nitalinda hadhi/heshima ya Shule na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe …….. Sahihi ya mwanafunzi ……

Mimi Mzazi/ Mlezi …….. Nimeshuhudia mtoto wangu
……..
akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi
kikamilifu katika kumlea kijana wangu naamini tutakuwa tunawasiliana.
Tarehe …….. Sahihi ya Mzazi/Mlezi
……..